

TANGAZO LA SERIKALI NA. 410 la tarehe 24/5/2024

**SHERIA YA KAMPUNI,
(SURA 212)**

NOTISI

(Imetolewachini ya kifungu cha 452A)

NOTISI YA MSAMAHA WA ADA YA UWASILISHAJI WA NYARAKA ZA KAMPUNI
NJE YA MUDA YA MWAKA 2024

KWA KUWA, kifungu cha 452A cha Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 kinatoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara, baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha kutoa msamaha wa ulipaji wa ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda;

NA KWA KUWA, lengo la kutolewa kwa msamaha wa ulipwaji wa ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda ni kuwezesha uhuishaji wa taarifa za kampuni kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao (Online Registration System) na kuuwezesha Mfumo huo kufanya kazi ipasavyo;

NA KWA KUWA, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara amepokea maombi ya kampuni kusamehewa kulipa ada ya kuwasilisha nyaraka za kampuni nje ya muda;

HIVYO BASI, MIMI ASHATU K. KIJAJI, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara, baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, kwa mujibu wa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 452A cha Sheria ya Kampuni, Sura 212 Niatoa Notisi ifuatayo:

Jina

1. Notisi hii itaitwa Notisi ya Msamaha wa Ada ya Uwasilishaji wa Nyaraka za Kampuni Nje ya Muda ya Mwaka 2024.

*Notisi ya Msamaha wa Ada ya Uwasilishaji wa Nyaraka za Kampuni
Nje ya Muda*

Tangazo La Serikali Na. 410 (Linaendelea)

Muda wa
kutumika

2. Notisi itanza kutumika kuanzia kwa tarehe ya itakayo chapishwa katika Gazeti la Serikali na itatumika kwa kipindi cha miezi kumi na miwili.

Msamaha

3. Msamaha wa asilimia hamsini (50%) ya ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda unatolewa kwa kampuni zenye maombi yanayokidhi vigezo vilivyoainishwa katika aya ya (4) ya Notisi hii.

Vigezo vya
msamaha

4. Msamaha wa ada ya uwasilishaji wa nyaraka za kampuni nje ya muda unatolewa kwa:

- (a) kampuni zilizosajiliwa kabla ya mwaka 2018, ambazo taarifa zake hazijahuishwa kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao;
- (b) maombi ya kuhuisha taarifa za kampuni yaliyopo kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao kabla ya tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii;
- (c) maombi ya kuhuisha taarifa za kampuni kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao yatakayopokelewa kwenye Mtandao ndani ya muda wa Notisi hii; na
- (d) malipo yanayokidhi vigezo vya (a), (b) au (c) yatakayolipwa ndani ya muda wa Notisi hii.

Dodoma,
13 Mei, 2024

ASHATU K. KIJAJI
Waziri wa Viwanda na Biashara